



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA NISHATI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA  
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI  
(EWURA)



## TAARIFA KWA UMMA

### MWITO WA KUTOA MAONI YA WADAU KUHUSU KUBADILISHA KANUNI NDOGO ZA KUKOKOTOA BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA

EWURA imepokea maombi kutoka kwa Wafanyabiashara wa Jumla wa Mafuta (OMCs) ya kurekebisha gharama za kibenki za uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli kutoka asilimia 1 mpaka asilimia 2.5 pamoja na viwango vya kubadilishia fedha za kigeni vinavyotumika katika kukokotoa bei kikomo ya mafuta ya petroli.

Kwa mujibu wa kifungu cha 19(2) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414, EWURA imeanzisha taftishi ili kukusanya maoni ya wadau kuhusu kurekebisha gharama za kibenki zinazohusiana na uagizaji wa bidhaa za mafuta ya petroli na kurekebisha kanuni za ukokotoaji wa bei ili viwango vya kubadilishia fedha za kigeni.

EWURA inakaribisha wadau wote kutoa maoni ya maandishi kuhusu pendekezo lililoletwa na Kampuni za Mafuta kwa kuyawasilishwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kupitia anuani iliyotajwa hapa chini **ndani ya siku saba kutoka tarehe ya tangazo hili.**

Mkurugenzi Mkuu,  
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji,  
EWURA House, 3 EWURA Street, 41104 Tambukareli,  
S.L.P 2857,  
**DODOMA.**

Imetolewa na:  
**Mkurugenzi Mkuu**  
**Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**  
**18 Mei 2023**